Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Pili – Tarehe 9 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 11

**Ongezeko la Tatizo la Udhibiti wa Taka Ngumu**

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la tatizo la udhibiti wa taka ngumu hapa nchini jambo linalosababisha kuongezeka kwa taka hizo siku hadi siku ambazo hazizolewi kwa kiwango kisichozidi asilimia 50. Je, Serikali inaweza kueleza ugumu wa tatizo hili ni nini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli udhibiti wa taka ngumu nchini haujafikia kiwango cha kuridhisha. Hali hii imesababishwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi dhaifu wa sheria na kanuni zinazohimiza usafi wa mazingira mijini, pamoja na usimamizi hafifu wa wakandarasi wanaopata *tender* za usafi katika Majiji, Manispaa na Halmashauri zetu; ushiriki mdogo wa wananchi kuchangia gharama za uzoaji na utupaji taka; uchache na uchakavu wa vifaa na vitendea kazi kama vile magari na mitambo ya kushindilia taka kwenye madampo; uduni wa miundombinu kama vile maeneo ya kuweka taka kwa muda ili yaweze kusafirishwa katika dampo, lakini vilevile

barabara kwa ajili ya usafirishaji wa taka hizo; uelewa mdogo wa usafi wa mazingira kwa jamii na uzingatiaji duni wa wale wanaoelewa; na kukosekana kwa mkakati madhubuti wa kusimamia uzoaji na utupaji wa taka.

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti changamoto ya taka ngumu nchini, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na wadau wengineimeandaa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka. Mkakati huu umechambua upungufu uliopo wa usimamizi wa taka na hivyo umeainisha hatua muhimu za kuchukuliwa katika vipindi vya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Aidha, Serikali itaanza kutekeleza miradi kadhaa ili kudhibiti tatizo la taka ngumu nchini. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Kuandaa Mpango wa Kuboresha Mazingira Katika Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Manispaa ya Arusha, ambayo tunategemea kuwa na *Environmental Master Plan*. Uandaaji wa Mpango huu ulianza mwezi Machi mwaka huu na utakamilika mwezi Desemba mwaka huu. Mradi huu unafadhiliwa na nchi yetu pamoja na Serikali ya Korea.

Mradi mwingine ni wa Kusafisha Mazingira ya Mto Msimbazi unaosimamiwa na *NEMC* kwa ufadhili wa *UNEP*. Hatua za awali zimeshaanza, ambapo Ujumbe kutoka *UNEP* umeshafanya ukaguzi kwenye eneo la Mradi.

Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, itatekeleza Mradi ujulikanao *Tanzania Strategic Cities Programme.* Huu ni Mradi wa miaka mitano na utaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha kuanzia 2010 hadi 2014. Mradi huu utatekelezwa katika miji minane nchini ambayo ni Mwanza, Arusha, Mbeya, Mtwara, Tanga, Kigoma na Dodoma na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu *(CDA).* Shughuli kubwa ya Mradi huu ni ukarabati na upanuzi wa miundombinu, ikiwa ni pamoja na suala la udhibiti wa taka ngumu. Mradi huu utatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia na ufadhili wa DANIDA.

Mheshimiwa Spika, taka ngumu ni mali iwapo usimamizi wake utaimarishwa. Kwa mfano, Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Korea, utakuwa na miradi ya kuzalisha nishati kutokana na taka ngumu. Aidha, taka ngumu zinaporejelezwa, bidhaa mbalimbali zenye manufaa huzalishwa.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa taka ni jukumu la kila mwananchi. Tuepuke kutupa taka ovyo ili kuboresha usafi katika miji yetu. Kila mmoja wetu awe msimamizi na mteteaji mkubwa na tukemee wale wanaochafua mazingira.

Napenda nichukue fursa hii, kuipongeza Manispaa ya Moshi na Jiji la Mwanza, ambao wamekuwa washindi wa zawadi ya mashindano ya afya na usafi wa mazingira inayotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kila mwaka tarehe 5 Juni wakati wa sherehe za Siku ya Mazingira Duniani. Aidha, napenda kuhimiza Halmashauri nyingine ziige mfano huu ili kuboresha usafi wa mazingira.

**MHE. MKIWA ADAM KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa ufadhili wa Serikali ya Korea unaonesha kwamba uzalishaji wa nishati kwa kutumia taka ngumu unaweza kuisaidia nchi yetu kuepukana na gharama kubwa za nishati; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati amelisema hili siku zilizopita: Je, suala hili la kutumia nishati kwa kutumia taka ngumu litaanza lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la ndugu yangu na dada yangu, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, utekelezaji wa utumiaji wa taka ngumu kwa ajili ya utengenezaji wa nishati umeshaanza na katika Jiji la Dar es Salaam tayari tuna Mradi wa Dampo la Mtoni, ambapo tunategemea kuanza hivi karibuni. Mradi huo utazalisha megawatt 2.5, ambapo itawauzia TANESCO na hatimaye kuweza kupata fedha kutokana na taka zile na gesijoto ambazo zingekuwa zinaenea angani.

Kwa hiyo, Mradi huo ni wa Nishati lakini vilevile utashirikishwa kwenye mpango mzima wa *Clean Development Mechanism,* ambayo inatokana na *Kyoto Protocol.* Nimueleze tu kwa hatua ya dampo hili la Jiji la Dar es Salaam, pamoja na Manispaa ya Mwanza na Arusha ni mradi wa majaribio na hatua za makusudi za Serikali ni kusambaza utaratibu huo katika maeneo yote ambayo yatakuwa na taka nyingi na madampo makubwa.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam limekithiri kwa taka ngumu kwenye maeneo ya masoko na hata majumbani; na kwa kuwa uchafu huo umekuwa ni kero kubwa sana na hatimaye kusababisha maradhi; je, Serikali ina mpango gani wa kuielimisha jamii nayo iweke mkakati wa kutumia taka hizo na kuzigeuza mbolea ambayo haina madhara yoyote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Pwani kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa kuna uchafu mkubwa wa taka ngumu hasa katika maeneo ya masoko yetu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipofanya ziara katika Jiji la Dar es Salaam, moja ya mambo aliyoyaagiza ni kuhakikisha kwamba taka zile zinatumika kwa ajili ya kutengeneza mbolea. Kwa hiyo, tayari hatua mbalimbali zimeshaanza kwa ushirikiano wa wenzetu wa Wizara ya Kilimo na TAMISEMI ili kuona fursa gani na uwekezaji gani unaweza kutumika.

Nniseme tu Elimu inaendelea na sisi wenyewe wananchi tuendelee kutoa Elimu katika ngazi mbalimbali. Ninapenda kutumia fursa hii, kuwapongeza wale wote ambao wamekuwa wakitoa Elimu na Taasisi mbalimbali za kijamii ambazo zimekuwa zikitoa Elimu na hasa Taasisi hii ya kijamii ambayo inaendeshwa na wanaharakati wa Sheria ya Mazingira, ambayo hivi sasa wanarusha matangazo katika televisheni ya kuonesha na kukemea tatizo zima la uchafu wa mazingira katika madampo na katika maeneo ya makazi yetu.

Na. 12

**Ruzuku kwa Dawa za Walemavu wa Ngozi *(Albino)***

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH (K.n.y. MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR**) aliuliza:-

Nchi yetu inawajali sana watu wa makundi mbalimbali ya walemavu nchini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku ya dawa za bure kwa ajili ya kundi la walemavu wa ngozi *(Albino*) nchini ili wapate dawa ya kujikinga na saratani ya ngozi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inaandaa utaratibu wa kununua dawa na kuzisambaza kwa ajili ya walemavu ngozi (*Albino*), kujikinga na Saratani ya ngozi katika mwaka wa fedha wa 2010/2011. Kwa kuanzia, dawa hizo zitasambazwa hadi Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya na Hospitali Teule kupitia Bohari ya Dawa. Mpango wa kuzifikisha dawa hizo hadi ngazi ya zahanati na vituo vya afya utafuata.

Mheshimiwa Spika, taarifa itatolewa kwa wananchi kuhusu namna ya kuzipata dawa hizi mara zitakaposambazwa katika Hospitali za Mikoa, Wilaya na Hospitali Teule ili waweze kuzitumia. Aidha, dawa hizi zitatolewa bila malipo kwa walemavu wa ngozi.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Pamoja na hizi dawa lakini tunaona kwamba walemavu wa ngozi wana matatizo wakati wanapoingia juani na macho yao kuyakunja kutokana na mwanga mkali wa jua. Je, Serikali ina utaratibu wa kuona kwamba kila mwenye ulemavu huu anapata miwani; chombo ambacho siyo ghali ili iweze kumsaidia?

(ii) Kwa faida ya Bunge hili na nchi yetu; sijui Mheshimiwa Waziri anaweza akatuambia kuna walemavu wa ngozi wangapi Nchini Tanzania?

**SPIKA:** La pili naona ni la takwimu, sijui linastahili wakati huu, lakini inategemea. Mheshimiwa Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Rished kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa wenzetu wenye ulemavu wa ngozi pia wanapata matatizo sana wanapopata mwanga machoni. Ninakubaliana kwamba, wanahitaji kabisa kupewa miwani, lakini vilevile kupatiwa kofia za kuwakinga ili jua lisiweze kuwapata.

Kwa hiyo, sisi kama Wizara tunalichukua hili ili tuweze kuona kwamba ni namna gani wakati tunatoa dawa za ngozi, tuweze kuwapatia miwani ambazo wataweza kuzipata japo kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la idadi ya watu wenye ulemavu wa ngozi, Wizara sasa hivi kwa kweli haina taarifa ambayo ni ya uhakika. Tumefanya Sensa Maalum ambayo itatuwezesha kujua idadi ya *albino* ambao wapo kuanzia ngazi ya Mikoa, Wilaya mpaka katika Vitongoji.

Kwa hiyo, mara tu tutakapomaliza zoezi hili, basi tutakuwa katika hali nzuri ya kutoa takwimu ambazo zitakuwa ni sahihi zaidi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa swali linahusu Serikali kuwajali sana watu wa makundi mbalimbali ya ulemavu; na kwa kuwa watoto wengi wenye ulemavu wa viungo wanashindwa kwenda shuleni kutokana na kutokuwa na vifaa vya usafiri; je, Serikali kupitia Wizara ya Afya ina mpango wowote wa kuwasaidia watoto wa aina hiyo ili kuongeza watoto wenye ulemavu shuleni?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli watu wenye ulemavu wa viungo wanapata shida sana ya usafiri. Sasa hivi Wizara ya Afya hatuna uwezo wa kuweza kumnunulia chombo cha usafiri kila mwenye ulemavu wa viungo, isipokuwa kuna wachache ambao kupitia Ustawi wa Jamii, wameweza kusaidiwa na kupatiwa vyombo hivyo. Kwa hiyo, hatuwezi kuahidi lakini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao wanajitolea kusaidiana na sisi kama Serikali, tutakapokuwa na uwezo tunaweza tukawapatia usafiri. Kwa sasa hatuwezi kuahidi kwamba, kila mlemavu wa viungo hasa watoto tutawapatia usafiri wa kwenda shule.

Na. 13

**Madhara ya Ugonjwa wa Saratani**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Ugonjwa wa Saratani unaua watu wengi zaidi kuliko hata UKIMWI; je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Juma Said Omar kuwa, Saratani inaua watu wengi zaidi duniani kuliko UKIMWI. Takwimu za Shirika la Afya Duniani zinaonesha kwamba, Saratani inaua watu wengi hususan katika nchi zinazoendelea Tanzania ikiwa ni nchi mojawapo. Inategemewa kwamba, ifikapo mwaka 2020, theluthi mbili ya vifo vyote vitakavyosababishwa na Saratani duniani vitatokea katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa Mkakati wa Kukabiliana na ongezeko hili la Ugonjwa wa Saratani. Mkakati huu unajumuisha mipango ifuatayo:-

Kwanza, Mpango wa Kuzuia Saratani unaolenga kutoa elimu ya namna ya kuepuka vitu vinavyosababisha Saratani, kwa mfano, matumizi ya bidhaa za Tumbaku. Aidha, Wizara imeanzisha huduma ya kuwapima wananchi wakiwa hawana dalili (*Cancer Screening*) ili kugundua Saratani kabla haijapevuka.

Pili, kutoa huduma za ugunduzi wa Saratani mapema wakati bado inatibika na kupona. Bahati mbaya, zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wanakuja hospitali Saratani ikiwa katika hatua ngumu ya kutibu.

Tatu, kuboresha matibabu kwa kupanua Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* na kuanzisha vituo vingine vya Saratani katika Hospitali nyingine za Kanda (Bugando, KCMC na Mbeya) na Hospitali za Mikoa, kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Nne, kutoa Tiba Shufaa (*Palliative Care*) kwa wagonjwa ambao wako katika hatua za mwisho za ugonjwa ambapo matibabu ya kuwaponyesha yameshindikana.

Tano, kuongeza idadi ya Wataalamu katika fani hii kwa kuanzisha kozi ya Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Saratani katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili (MUHAS). Mafunzo haya yataanza mwezi Septemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, mipango yote hiyo ni ya muda mrefu na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hivi sasa upanuzi wa Taaasisi ya Saratani ya *Ocean Road* unaendelea. Aidha, ujenzi wa Kituo cha Matibabu ya Saratani katika hospitali ya Bundando pia unaendelea.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa wananchi walio wengi hawaelewi kuhusu ugonjwa huu; je, Serikali inawaambia nini wananchi kuhusu chanzo na kinga dhidi ya Ugonjwa huu wa Saratani?

(ii) Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuwa miongoni mwa waathirika wa Ugonjwa huu; je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuwafanyia uchunguzi Wabunge wote kabla ya kumaliza Bunge hili na kuhakikisha usalama wao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Juma Said Omar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya wananchi bado hawaelewi chanzo na kinga ya Saratani. Wizara yangu kwa kutumia vyombo vya habari na vipeperushi, tumekuwa tukitoa Elimu kwa watu ili kuweza kuwaambia kwamba, tatizo la Saratani lipo na linasababisha vifo vingi. Chanzo katika baadhi ya Saratani nyingi hakijaweza kufahamika, isipokuwa kuna vitu ambavyo vinashabihiana ambavyo vinaweza kuleta tatizo la Saratani na Elimu ya kinga ya Saratani pia inaweza ikatolewa ili kuweza kujua matumizi ya vile vitu ambavyo vinasababisha kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba, utumiaji wa Tumbaku unasababisha Saratani. Kwa hiyo, hizi ni Elimu tulizotoa, pamoja na kujiangalia kwa kwenda hospitali kupata ushauri wa Wataalamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mkusanyiko wa watu wengi hasa kama sisi Waheshimiwa Wabunge tuliopo hapa, siyo kitu cha ajabu kuona baadhi yetu wengine wana matatizo ya Saratani.

Tunachoweza kufanya ni kwamba, pamoja na elimu tunayotoa, lakini Wizara ya Afya wakati wa vikao vya bajeti tulikuwa tukileta wataalamu ambao huwa wanafanya *screening* au wanatoa elimu na uchunguzi kwa Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kugundua japo dalili za mapema ambazo zinaweza kuelezea kama mtu anaweza kuwa na Saratani. Labda tu niseme, tutakaa tuweze kuona katika muda huu wa Bunge kama tutaweza kuwaleta wataalamu kwa sababu wenzetu wa MEWATA walishafika hapa, lakini pia madaktari kutoka Muhimbili walishawahi kuja hapa na waliweza kufanya vipimo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na matatizo mengine ya *cancer* kwa Waheshimiwa Wabunge Wanaume. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hivi majuzi tu kuna chombo kimoja cha habari kilimwonesha mtoto mdogo ambaye anasumbuliwa na Saratani *serious* yuko Zanzibar, Bububu Hospital; na kwa kuwa inaonekana kwamba yule mtoto familia yake haina uwezo na ikaomba watu ama Serikali isaidie; je, Serikali itakubaliana nami kwamba imsaidie mtoto yule ili apelekwe India au Marekani akafanyiwe matibabu ya haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Tanzania Bara, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ya Zanzibar, tumekuwa na mahusiano mazuri sana katika kutoa tiba, ikiwa ni pamoja na zile za rufaa kwa wagonjwa mbalimbali. Bahati mbaya mimi sikuona jana walipokuwa wanamuonesha huyo mtoto kutoka Bububu, lakini ninachoweza kusema hapa ni kwamba, mtu yeyote anapoumwa anakwenda kwa daktari na madaktari ndiyo wanaofanya rufaa. Kwa hiyo, mimi nashauri kuwa, wale wenzetu wa Zanzibar, kama wamemwona huyo mtoto anahitaji kupata rufaa ni vizuri tukashirikiana ili aweze kufuata taratibu zote za rufaa hatimaye aidha atibiwe pale *Ocean Road* au apelekwe nje.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiona wagonjwa wengi sana kutoka Zanzibar, wengine wamekuwa wakitibiwa wakiwa hapa Tanzania, lakini wengine pia tumeweza kuwapa rufaa kwenda nje ya nchi. Kwa hiyo, naomba tushirikiane ili tuweze kuhakikisha kwamba, si huyu mtoto tu, lakini hata mwingine mwenye matatizo haya aweze kupewa ushauri na matibabu kama inawezekana. *(Makofi)*

Na. 14

**Mpango wa Kuvipatia Maji Vijjiji vya Matongo na Isene**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishaahidi kwa muda mrefu kuvipatia huduma ya maji Vijiji vya Matongo na Isene ambavyo mpaka sasa havina maji na wakati wa kiangazi wananchi hufuata maji kwa umbali wa takriban kilomita sita:-

Je, mpango wa kuwapatia wananchi hawa maji bado upo na utatekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2007/2008 na 2008/2009, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ilitekeleza miradi midogo ya maji inayoweza kutoa matokeo ya haraka maarufu kama *Quickwin Schemes* katika Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira.

Vijiji 13 vilivyopewa kipaumbele ni Nyahaa, Mkalama, Kidarafa, Gumanga, Kikhonda, Mutamba, Iguguno, Nguvumali, Mugungia, Ujungu, Mlandala, Ng'ang'uli na Mingela. Vijiji vya Matongo na Isene havikujumuishwa katika utekelezaji wa mradi kwenye awamu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo la upatikanaji wa maji katika Kijiji cha Matongo, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, imetenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya kuchimba kisima kirefu. Uchunguzi wa maji chini ya ardhi tayari umekamilika na mpango kazi uliopo ni kuchimba kisima kirefu mwezi huu wa Juni, 2010. Aidha, katika mwaka 2010/2011, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, imepanga kutumia shilingi milioni 300 kuchimba visima katika vijiji saba vya Isene, Senene, Kinyambuli, Mseko, Munguli, Kizonzo na Kikonge.

Kwa maelezo haya, naiomba Halmashauri ya Wilaya ya Iramba itoe kipaumbele kwa Vijiji vya Matongo na Isene na kunipa taarifa ya utekelezaji.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa toka Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne ya Utawala wa Nchi hii, Serikali imeweka mkazo sana kuwasaidia Watu wa Iramba Mashariki kupata maji:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kupokea salamu kutoka kwa Wananchi wa Iramba Mashariki?

(b) Kwa kuwa kazi ya uchimbaji wa kisima katika Kijiji cha Matongo itaanza mwezi huu wa Sita; Serikali itakuwa tayari sasa kuhimiza ili mwaka mpya wa fedha unapoanza na vijiji vilivyobaki vipatiwe maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naona la kwanza siyo swali ni kupokea salamu na nimezipokea kwa niaba ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, bila shaka ametambua utekelezaji wetu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Iramba.

Swali la pili kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, mwisho kabisa nimesema, naiomba Halmashauri ya Wilaya ya Iramba ijipange vizuri kutekeleza miradi katika vijiji saba nilivyovitaja na kufuatilia hizi shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuchimba visima katika vijiji hivyo saba. Ninamuahidi Mheshimiwa Msindai kwamba, tutaendelea kusukuma suala hili katika msimu ujao, hata kama hatutakuwepo katika Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imekubali kupeleka maji kwenye vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mgana Msindai; na kwa kuwa hata vijiji ambavyo tayari vina maji bado Serikali haijasambaza maji kwenye makazi; je, Mradi huo alioutaja Mheshimiwa Naibu Waziri utaambatana na kazi ya kupeleka maji kwenye makazi ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji unakamilika pale ambapo wananchi wanapata huduma ya maji. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba, kazi mojawapo ambayo tutaifanya ni kuangalia uwezekano wa kuwafikishia wananchi maji katika mwendo mfupi, mara nyingi tunasema angalau mita 400 kutoka pale walipo.

Kwa hiyo, hii ndiyo kazi ambayo iko mbele yetu na ninamhakikishia Mheshimiwa Chilolo kwamba, kazi ya usambazaji maji pia ni jukumu letu.

Na. 15

**Mgogoro Kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Wananchi**

**MHE. DAMAS PASCAL NAKEI** aliuliza:-

Mgogoro kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Wananchi wa Vijiji vya Gijedabung, Gedamar na Ayamango ni wa siku nyingi zaidi ya miaka thelathini. Kutokana na amri ya Mahakama, Wananchi wa Vijiji hivyo walitakiwa wapatiwe eneo mbadala la hekta 8,000 na kulipwa fidia, kitu ambacho Serikali imeshindwa kutekeleza:-

Je, Serikali haioni kwamba kutolipatia ufumbuzi tatizo la mgogoro huo ni kuhalalisha matumizi ya maeneo hayo ili wananchi waendelee na maisha yao ya kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli mgogoro kati ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Wananchi wa Vijiji vya Gijedabung, Gedamar na Ayamango ni wa siku nyingi, kama Mheshimiwa Mbunge alivyobainisha. Mgogoro huo unatokana na Wananchi wa Vijiji hivyo vilivyoanzishwa kati ya mwaka 1976 na 1992 kutakiwa kuondoka ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, iliyokuwa tayari imetangazwa rasmi kuwa Hifadhi ya Taifa kupitia Gazeti la Serikali Namba 160 la Mwaka 1970, jambo ambalo wananchi hao hawakulitekeleza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004, *TANAPA* ilifanya zoezi la kuhakiki mipaka ya Hifadhi zake kwa kuwatumia Wataalamu wa Idara ya Upimaji na Ramani kutoka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na kuwashirikisha wadau wote katika kubainisha mipaka ya Hifadhi. Baada ya zoezi hilo la kutambua mipaka ya Hifadhi ardhini kukamilika, ilibainika kuwa, jumla ya Kaya 244 za vijiji vilivyotajwa, zilikuwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, taarifa ambayo iliwasilishwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara Januari, 2005, ambaye aliunda Kamati iliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Babati, kushughulikia mgogoro huo na kuwasilisha mapendekezo ya utatuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitoa mapendekezo na kati ya hayo ni kuhamishwa kwa wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi. Mkuu wa Mkoa alikubaliana na mapendekezo hayo na kutoa agizo kwa wananchi hao kuwa wawe wameondoka katika eneo hilo ifikapo tarehe 31 Agosti, 2006. Hata hivyo, wanavijiji hao hawakutekeleza agizo hilo kwa muda na badala yake walifungua Kesi Namba 23 ya 2006 ya Madai ya Ardhi katika Mahakama Kuu ya Tanzania (Arusha), Kitengo cha Ardhi, dhidi ya Bodi ya Wadhamini ya *TANAPA*.

Mwezi Mei, 2008, kwa hiari yao wenyewe, Wenyeviti wa Vijiji husika, walipeleka ombi la kufuta kesi hiyo. Mahakama Kuu ilikubali ombi hili na kesi iliondolewa tarehe 15 Septemba, 2008 kwa masharti yafuatayo: Wananchi wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi waondolewe, wapewe ardhi mbadala na walipwe fidia ya nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo la Mahakama, Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilianza kutafuta ardhi mbadala. Bodi ya Wadhamini ya *TANAPA* ilikubali na iliidhinisha kiasi cha shilingi 175,050,942 kwa ajili ya kulipa fidia ya nyumba za wanavijiji hao.

Hata hivyo, ni kijiji kimoja tu cha Gjedabung ndicho kilikubali na kulipwa jumla ya shilingi 37,175,332 kwa Kaya 51. Utaratibu wa malipo ya fidia kwa kaya zingine 23 zilizosahaulika katika tathmini ya awali katika Kijiji cha Gjedabung nao tayari umekamilika na shilingi 19,514,940 za nyongeza zimetengwa.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Ayamango na Egedamar vilikataa kuondoka katika Eneo la Hifadhi vikisubiri kupatiwa eneo mbadala. Mpaka sasa Wilaya ya Babati imekwishapata Eneo la Kiongozi (Babati Mjini), ambalo linaweza kupokea Kaya 50. Pia Halmashauri imeainisha maeneo mengine ya mashamba ambayo hayatumiki likiwemo Shamba la Galapo na tayari yamekwishatolewa maombi kwa Mheshimiwa Rais ili kufuta *tittle* ya maeneo hayo na kuyarudisha Serikalini ili yagaiwe kwa wanavijiji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona kuwa si vyema na ni kinyume cha taratibu na kukiuka amri ya Mahakama kama itawaruhusu wanavijiji hao kuendelea kuishi ndani ya eneo la Hifadhi na kuendelea kuharibu mazingira.

Hali hiyo itasababisha kuharibika kwa vyanzo vya Mto Tarangire vilivyopo ndani na nje ya Hifadhi hiyo. Kwa hiyo, *TANAPA* imekwishatenga pesa za kulipa fidia za

nyumba za wanavijiji hao wakati Halmashauri inaendelea kufuatilia upatikanaji wa maeneo mbadala.

**MHE. DAMAS PASCAL NAKEI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo hayajaleta mafanikio hadi sasa; mwaka jana katika Bunge hili Mheshimiwa Waziri aliahidi kutembelea eneo lile na kuonana na wananchi wa maeneo hayo na aliahidi kwamba, angefanya hivyo kabla ya Bunge la Mwezi wa Kumi mwaka jana na hakuweza kufanya hivyo; Bunge la Februari hakuweza kufanya hivyo hadi Aprili na mpaka sasa; je, sasa ni lini Waziri atakuja kutekeleza ahadi yake ambayo aliitoa humu Bungeni tukizingatia kwamba muda uliobaki ni majuma manne tu?

Je, yuko tayari tuongozane naye katika muda wa siku mbili, tatu, zijazo ili kuonana na wananchi hao?

**SPIKA:** Si vizuri mkaondoka kesho wakati ambapo Bajeti inasomwa, labda baadae kidogo. Mheshimiwa Naibu Waziri! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nakei, Mbunge wa Babati Vijijini, kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Waziri alikubali maombi ya Mheshimiwa Mbunge kwamba, atembelee eneo hilo kwa ajili ya kuwaelekeza wananchi nini kinachoendelea. Niseme tu kwamba, wakati mwingine tunapata tabu kidogo tunapokuwa na *strict preferences,* kwa sababu katika maombi ya Mheshimiwa Mbunge, alisisitiza kwamba ni muhimu Mheshimiwa Waziri mwenyewe, kitu ambacho kimeleta tabu kidogo kwake yeye mwenyewe kutokana na majukumu mengine mengi ambayo yamekuwa yakimkabili. Kwa hiyo, nilikuwa napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, pengine itakuwa ni kwa manufaa ya Wananchi na manufaa ya Taifa, akilegeza sharti hilo ili maafisa wengine wa Wizara akiwemo Katibu Mkuu, hata mimi mwenyewe, tuweze kwenda; kazi ambayo kikatiba tunapaswa kuifanya na tuko tayari.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika maelezo yake Naibu Waziri alianzia historia ya mgogoro huu mwaka wa 1972 lakini akaacha kueleza tatizo la msingi la watu hawa walitokea wapi; na kwa kuwa wananchi hawa walitokea Vijiji vya Gawal, Gidgarmod, Murjanda, *Basotu Plantation* na maeneo mengine ambayo baadae yakageuka kuwa *Tanzania Canada Wheat Complex* kule Hanang; na kwa kuwa wananchi hawa waliondolewa na Serikali kwa nguvu kupisha mashamba ya ngano na sasa mashamba hayo yameshindikana na eneo hilo limebinafsishwa kwa watu binafsi; kwa nini watu hawa ambao waliondolewa kwenye maeneo yao Serikali inachukua muda mrefu hivi kuwapatia maeneo ya uhakika kwa haraka ili kuwaondoa katika hali ya kuishi kama wakimbizi katika nchi yao wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo lipo ni taratibu na sheria, wakati mwingine ukivunja sheria unajikuta unafanya makosa zaidi ndiyo maana Halmashauri ya Wilaya ya Babati imekuwa ikitafuta maeneo. Katika orodha ya maeneo mbalimbali ambayo yameainishwa kwa ajili ya matumizi ya wananchi hao ni pamoja na eneo la *Galakwe Estate,* lakini yako pia maeneo mengine.

Sasa maeneo haya yana *tittles* za watu na Sheria inasema *tittle* ya mtu inakuwa *revoked* na Mheshimiwa Rais na mchakato wa kufanya hivyo unaendelea. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri ni vizuri wananchi wakawa wavumilivu, Wizara na Serikali inafanya hivi si kwa makusudi lakini ni kujaribu kufuata taratibu ambazo tumejiwekea ili kuepusha matatizo mengine makubwa zaidi ambayo yanaweza yakajitokeza kutokana na kuvunja sheria.

Na. 16

**Ruzuku ya Mbolea na Mbegu**

**MHE. PASCHAL CONSTANTINE DEGERA** aliuliza:-

Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa ruzuku kwenye kilimo nchini ikiwemo ruzuku ya mbolea na mbegu ambayo hutolewa kwa mikoa michache nchini:-

Je, ni mikoa ipi inayonufaika na ruzuku hiyo; na ile mikoa ambayo haipati ruzuku hiyo inafaidika vipi hasa ikizingatiwa kuwa, fedha za ruzuku hiyo zinatokana na kodi za Watanzania wote?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Constatine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Jumla ya Mikoa 20 ya Tanzania Bara inanufaika na mpango wa ruzuku. Kati ya mikoa hiyo, Mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Kigoma, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mara (Wilaya za Tarime na Serengeti), Tabora (Wilaya za Sikonge na Urambo), Shinyanga (Wilaya za Kahama na Bukombe), Kagera (Wilaya ya Chato), Mwanza (Wilaya za Geita na Sengerema) na maeneo yenye miundombinu ya umwagiliaji iliyokamilika ya Mikoa ya Mtwara (Wilaya ya Mtwara), Lindi ( Wilaya ya Lindi), Tanga (Wilaya ya Korogwe, Muheza na Lushoto), Dodoma (Wilaya ya Mpwapwa na Bahi), Pwani (Wilaya ya Bagamoyo), Singida (Wilaya ya Manyoni na Singida), Mara (Wilaya

ya Bunda) na Tabora (Wilaya ya Igunga), ilinufaika na ruzuku ya mbolea na mbegu bora za mahindi na mpunga. Lengo la ruzuku hiyo ya mbolea na mbegu bora ni kuongeza tija za uzalishaji wa mazao ya chakula nchini.

Mikoa ya Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora na Dodoma imenufaika na ruzuku ya mbegu bora za mtama na Mikoa ya Dodoma, Singida na Shinyanga imenufaika na ruzuku ya mbegu bora za alizeti.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kigoma (Wilaya za Kasulu na Kibondo), Manyara (Wilaya ya Babati), Singida (Wilaya ya Manyoni, Singida na Iramba), Tabora, Morogoro na Iringa (Wilaya ya Iringa), imenufaika na ruzuku ya mbegu za pamba na madawa.

Ruzuku ya miche bora ya zao la chai hutolewa katika maeneo yanayozalisha zao hilo kwa wingi, ambayo ni Iringa, Mbeya, Kagera, Mara na Tanga. Ruzuku ya miche bora ya kahawa hotolewa kwa wakulima wa zao hilo katika Mikoa ya Ruvuma (Mbinga na Songea), Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Rukwa, Arusha (Arumeru, Monduli na Karatu), Tanga, Iringa (Njombe, Ludewa na Kilolo), Kigoma na Mara.

Aidha, wakulima wanaozalisha Zao la Korosho katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma (Tunduru), Tanga, Kagera (Chato), Kilimanjaro, Morogoro (Kilosa) na Mbeya (Kyela), hupata ruzuku ya madawa ya kudhibiti visumbufu vya zao hilo la wakulima wa pamba katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kigoma (Kasulu na Kibondo), Manyara (Babati), Singida (Manyoni, Iramba na Singida), Tabora, Morogoro, Iringa (Iringa) na Kagera (Chato), hupata ruzuku ya viuatilifu vya kudhibiti visumbufu vya zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ruzuku umesaidia sana katika kuongeza usalama wa chakula nchini. Ziada inayozalishwa katika maeneo yaliyopatiwa ruzuku, hupelekwa katika maeneo ambayo hukabiliwa na hali ya ukame wa mara kwa mara, ukiwemo Mkoa wa Dodoma.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Mkoa wa Dodoma unapata ruzuku ya mbegu ya alizeti na kwa kuwa mpaka hivi sasa Wilaya ya Kondoa bado hatujawahi kuletewa mbegu ya alizeti yenye ruzuku. Je, ni lini Wilaya hiyo itapatiwa mbegu ya alizeti yenye ruzuku?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ziada ya mazao yanayozalishwa katika mikoa ambayo inapata ruzuku ya mbolea na mbegu inapelekwa katika mikoa kame ikiwemo Mkoa wa Dodoma na kwa kuwa Mkoa wa Dodoma una mabonde mazuri sana ya umwagiliaji, kwa nini

Serikali isiamue kuyaendeleza haya mabonde ili wakulima wa Dodoma nao wajitegemee badala ya kutegemea chakula kutoka mikoa hiyo ya ruzuku ikiwemo na bonde la Mto Bubu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama Wilaya ya Kondoa ni moja ya Wilaya ambazo zinalima vizuri alizeti basi Wilaya hii nayo inastahili kupatiwa ruzuku ya mbegu za alizeti. Tutatuma wataalam waweze kuangalia na kufuata vigezo ambavyo vinaashiria kwa Wilaya kupewa ruzuku hiyo ya mbegu za alizeti.

Pili, kuhusiana na kuendeleza mabonde hayo kwa ajili ya umwagiliaji hili ni suala la kitaalam, wataalam wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji wamesikia na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imesikia, kwa hiyo ni suala la kufuatilia, kuangalia kama uwekezaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika maeneo hayo italeta tija na ni kiasi gani cha fedha pamoja na masuala mengine ya upembuzi na kadhalika.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, naomba niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuleta mkakati huu wa kutoa ruzuku ambao ni kwa faida kwa Tanzania wakulima, hata hivyo nina swali fupi. Je, Serikali imefanya utafiti wa kutosha, wa kina na kujua kasoro zilizojitokeza katika utekelezaji wa mkakati huo ambao una nia nzuri sana kwa Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Dada yangu Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo.

**SPIKA:** Unasahihishwa na Mzee John Malecela anasema ni mama yako. *(Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kule nyumbani Anne Kilango Malecela ni dada yangu lakini kwa sababu Mzee Malecela amemwoa basi yeye ni shemeji yetu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwanza napenda kupokea pongezi za Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba Serikali inatoa ruzuku na kwa kweli ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwa na usalama wa chakula. Lakini katika mazao yale ya biashara vile vile Serikali inasaidia kusudi wananchi waweze kuongeza tija ya mazao hayo ili tuweze kupata mazao mengi ya kutumia humu nchini lakini kuuza nje ya nchi. Kasoro za mfumo huu kwa kweli zimeshafanyiwa utafiti na tumeshazifahamu na Mheshimiwa Malecela nakuhakikishia kwamba mwaka huu unaoanza 2010/11, kasoro nyingi zitakuwa zimepunguzwa. Lakini niombe tu kwamba katika Wilaya zile ambazo mfumo huu wa ruzuku unatekelezwa kwa kweli tunaomba tushirikiane na viongozi wote wa Chama na Serikali wakiwemo Mheshimiwa Malecela katika eneo lako ili tuweze kuhakikisha kwamba kwa kweli ruzuku hii inakwenda kwa walengwa na sio watu ambao hawahusiki.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Serikali katika huu mpango wa kilimo kwanza pamoja na ruzuku ya mbolea imesababisha wananchi wengi wamekuwa na moyo mkubwa wa kuwa wakulima, lakini tatizo ni moja tu kwamba, hii mbolea haijasambazwa katika Wilaya zote za Tanzania. Napenda kufahamu ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba hii ruzuku ya mbolea inasambaa katika Wilaya zote za Tanzania ikiwemo Wilaya ya Rorya, Musoma pamoja na Bunda?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kila Wilaya ingependa ipate ruzuku. Lakini niseme kwamba mahitaji halisi ya mbolea nchini ni takriban tani 385,000 na uwezo wa Serikali ni kutoa ruzuku katika maeneo yale ambayo yanazalisha chakula kusudi kuwe na usalama wa chakula. Nadhani mnakumbuka kabisa kwamba mwaka 2007/2008, tulitoa shilingi bilioni 61 kwa ajili ya mbolea na mbegu. Mwaka 2008/2009, tulitoa shilingi bilioni 96 kwa ajili ya ruzuku na mwaka huu tunatarajia kutoa shilingi bilioni 126 kwa ajili ya kutoa ruzuku ya mbolea na mbegu.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kupanga ni kuchagua. Kama bajeti uliyonayo haikuruhusu kutoa katika maeneo ya nchi nzima basi tunaangalia maeneo ambayo ni *priority* kwa ajili ya kuongeza usalama wa chakula nchini. Lakini kwa sasa hivi ni mikoa yote ambayo inapata ruzuku. Wengine wanapata ruzuku kwa ajili ya kilimo cha mahindi na mpunga wengine kwenye pamba, chai, kahawa na korosho. Kwa hiyo, nchi nzima kwa kweli imeguswa na ruzuku hii.

Na. 17

**Kuanzisha Vituo vya Wanyamakazi na Vya Kukodisha Matrekta Nchini**

**MHE MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Katika juhudi za kuboresha matumizi ya zana za kilimo nchini Serikali iliahidi kuwa itatimiza uanzishaji wa vituo vya wanyama kazi na kukodisha matrekta nchini; hasa katika ngazi za Halmashauri ya Wilaya:-

Je, ni vituo vingapi vimeanzishwa hadi sasa na katika Halmashauri zipi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ilianza kukarabati vituo vya wanyamakazi mwaka wa 2002/2003 na hadi kufikia mwaka huu wa

2009/2010 jumla ya vituo vya wanyamakazi 78 vimekarabatiwa katika Halmashauri za Wilaya 78 na orodha hiyo nimeshampatia Mheshimiwa Mbunge.

Aidha, kuanzia mwaka 2008/2009 jumla ya vituo vipya 10 vya wanyamakazi vimejengwa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *DADPs* inayotekelezwa chini ya Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini *ASDP*. Vituo hivyo vimejengwa katika Halmashauri za Wilaya za Tarime, Mvomero (Melela na Milama), Mkuranga (Mandimpera), Rufiji (Nyamwage), Mbinga (Utiri), Iramba (Gumanga) na Mkinga (Kichangani), Bagamoyo (Ubena Zomozi) na Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo kuanzia mwaka 2003/2004 imewezesha sekta binafsi kuanzisha vituo vitano vya kukodisha matrekta. Vituo hivyo viko kwenye Halmashauri za Wilaya za Songea ambacho kina matrekta matano na zana zake (Kituo hiki kinamilikiwa na Kanisa Katoliki Songea); Masasi ambacho kina matrekta matatu na zana zake (Kituo kinamilikiwa na Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Masasi); Singida ambacho kina matrekta matatu na zana zake (Kituo kinamilikiwa na KKKT Dayosisi ya Kanda ya Kati); Magu yenye vituo viwili kila kimoja kina matrekta matatu na zana zake na Maswa ambako kuna kituo kimoja chenye matrekta matano na *Power Tiller* 10 na zana zake.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mwito kwa wafanyabiashara na Taasisi nyingine kuanzisha vituo zaidi katika maeneo mbalimbali nchini na kuomba mikopo katika Taasisi za fedha, ili kuendeleza na kupanua huduma ya matumizi ya zana kwa wakulima.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri kwa jibu lake zuri ambalo amelitoa, lakini nina swali dogo tu. Wote tunajua Kanda ya Ziwa ni ya wakulima na wafugaji. Kuhusu miradi 10 hii inayozungumziwa ya *DADPs* maeneo mengi yametajwa ambayo sio ya wafugaji hasa. Je, ni vigezo gani vimetumika kuvijenga hivyo vituo 10 ambavyo vingeweza kujulikana hivyo vigezo kwa Kanda ya Ziwa ili nao waweze kunufaika na na mradi huo wa *DADPs*.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa kwamba Kanda ya Ziwa ni eneo la wakulima na wafugaji. Aidha, miradi ambayo inatokana na *DADPs* inaibuliwa na wananchi kupitia kwenye vijiji vyao na kupeleka Wilayani kusudi fedha zile ziweze kutengwa. Kwa hiyo, hii ni miradi ambayo haipelekwi na Serikali moja kwa moja. Fedha zipo, lakini wananchi ndio wanaoibua miradi ile, wataalam wanakagua na kuona kama miradi hiyo inafaa ili fedha ziweze kutumika. Kwa hiyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa kwamba katika Halmashauri hizo ambazo anaona kuna miradi mizuri basi aweze kuongea na wananchi kuwashawishi kuona umuhimu wa kupeleka suala hilo katika Wilaya kwa ajili ya *DADPs*.

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nataka niishukuru Serikali kwa

sababu ya kuleta haya matrekta madogo ambayo yanaitwa *Power Tillers* kwa wingi sana nchini. Lakini je, Serikali inayo habari kwamba wale wanaoleta haya matrekta hawaleti spea, kwa hiyo baada ya muda kama hatukuangalia matrekta mengi yatakuwa yamekaa bure kwa sababu spea hazipatikani? Je, Waziri anaweza kulihakikishia Bunge hili kwamba suala hilo litafuatiliwa kwa nguvu sana ili lisiwakatishe tamaa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa niaba ya Serikali napenda kupokea pongezi alizozitoa kwa ajili ya kuingiza *Power Tillers* kwenye Halmashauri zetu. Niseme kwamba nakubaliana naye kabisa kwamba kama Makampuni yanayouza *Power Tillers* hizi hayakuleta vipuri vya kufanyia *service* basi maana yake ni kwamba wakulima hao watakata tamaa lakini pia wataingia hasara kwa sababu pia wametumia fedha nyingi sana za kununua. Namhakikishia Mheshimiwa kwamba tutafuatilia suala hili kwa Makampuni yote ambayo yanauza hapa nchini waweze kuingiza vipuri ili viweze kuwasaidia wakulima wetu kwa sababu wanatumia fedha nyingi sana.

Lakini vile vile napenda kuzishauri Halmashauri ambazo zinanunua matrekta zihakikishe kwamba zinawasiliana vizuri na vituo vyetu vinavyoangalia haya matrekta yanayofaa kwa sababu mengine yanakuwa sio mazuri, lakini kwa sababu hayakupitia *CAMARTEC*. Sasa tuna kituo chetu cha *CAMARTEC* ambacho ndicho kinachohakikisha kwamba matrekta haya yanafaa kwa ardhi ya Tanzania. Kama hayajapitia pale yakiwa ni mabovu basi itakuwa ni *responsibility* ya maofisa hao walioruhusu matrekta hayo ambayo hayajapimwa yakaonekana ubora wake yakanunuliwa.

Mwisho kabisa natoa wito kwa Makampuni ambayo yanaingiza matrekta hapa nchini yahakikishe kwamba yanaingiza vipuri vyake ili wakulima wasiteseke na vile vile kuingiza vipuri pia kunatangaza biashara zao, kwa hiyo wajaribu kuangalia hali hiyo.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza moja. Kwa kuwa bei ya kununua matrekta inazidi kuongezeka mwaka hadi mwaka na kwa kuwa trekta moja linagharimu shilingi milioni 40 ni sawa na kununua Maksai pea 40. Je, hatuoni kama ingekuwa ni jambo zuri Serikali kuweka nguvu zaidi katika wanyamakazi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mzindakaya kwamba matrekta ni ghali, lakini vile vile tuelewe kwamba ili uweze kuleta (*Green Revolution*) yaani Mapinduzi ya Kijani lazima tutumie zana za kilimo ikiwa ni pamoja na kutumia matrekta na zana zingine ambazo zinaweza zikalima kiasi kikubwa cha ardhi kwa wakati mfupi. Kwa hiyo naweza kumshauri Mheshimiwa Mzindakaya kwamba sisi kama Serikali tutaendelea kwa yote matatu jembe la mkono kwa kutumia Maksai pamoja na kutumia matrekta.

Na. 18

**Uchakavu wa Majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Mwanva yamechakaa sana kiasi cha kuhatarisha maisha na usalama wa watumiaji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo hayo ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza?

(b) Je, ni lini Serikali itatoa usafiri katika Chuo hicho kama inavyofanya katika vyuo vingine nchini?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza kielimu watumishi pamoja na walimu wa chuo hicho ndani na nje ya nchi kama inavyofanya kwa watumishi wengine wa vyuo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a), (b) na (c ) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba majengo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanva ni chakavu na kwa sababu hiyo Wizara yangu imepanga kuyafanyia ukarabati katika mwaka mpya wa fedha 2010/2011.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mpango wa kuvipatia usafiri Vyuo vyote vya Maendeleo ya Wananchi kwa awamu kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, vyuo vilivyo mbali zaidi na Makao Makuu ya Wilaya hupewa kipaumbele. Hivyo napenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira zamu yake ikifika atapata gari.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara ina mpango wa kuwaendeleza watumishi na walimu wa vyuo vyetu. Mpango huu hutegemea sana upatikanaji wa fedha. Katika watumishi walioendelezwa mwaka wa fedha 2009/10 mmoja alitoka Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanva na mwaka wa 2010/2011 Wizara ina mpango wa kumwendeleza mtumishi mmoja wa chuo hiki.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri nikiamini kwamba ahadi aliyoitoa ndani ya Bunge hili ataitekeleza. Hata hivyo nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa vile Waziri amekiri kwamba Chuo hiki kina tatizo sugu la usafiri na kwa kuwa amesema kwamba katika mwaka wa Fedha 2010/2011, Chuo hiki hakitaweza kupewa gari jipya. Swali, Je, Serikali ina mpango gani wa kukisaidia Chuo hiki kwa fedha za kukarabati gari bovu ambalo limekaa pale kwa muda mrefu ili walau liweze kutumika wakati wakisubiri gari jipya.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELE YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna gari ambalo ni chakavu sana ambalo liko katika Chuo hiki na tumepata makisio ya matengezo ambayo yanafikia shilingi milioni 7 ili litengemae. Tumeahidi kwamba kama fedha ikitoka mwezi huu tunatarajia kupeleka fedha za matengenezo ya gari hili ambalo najua kwamba hata kama tutatoa hizi milioni saba litatembea kwa muda na litakuwa linasumbua zaidi. Lakini kwa sababu gari lipo na kwa sababu tumeshaliweka kwenye makisio Mheshimiwa Mbunge naomba avute subira, tukipata hela mwezi huu basi tutawapelekea katika Chuo chao.

Na. 19

**JWTZ Kuvamia Eneo la Wananchi Mwibara**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI (K.n.y. MHE. CHARLES M. KAJEGE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) limevamia eneo kubwa la kilimo linalotumiwa na zaidi ya vijiji vinne (4) vya Kata za Kibara na Nansimo katika Jimbo la Mwibara na kusababisha usumbufu mkubwa na njaa kwa raia:-

(a) Je, kuna mabadiliko yoyote ya kisera katika Jeshi hilo ambayo yanasababisha kutumia vitisho na mabavu ya kunyang'anya wananchi ardhi yao?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha Jeshi kuvamia eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kajege, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Eneo la Mlima Vunere limeainishwa kuwa eneo la Hifadhi ya Taifa. Kwa kutambua hilo Afisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda aliweka alama umbali wa mita sitini (60) toka kwenye kingo za mlima Vunere kuzuia wananchi wasiendelee kuingia zaidi na kulima eneo la hifadhi. Sheria zinazuia eneo la Hifadhi kutumiwa kwa shughuli za kudumu ikiwemo kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kajenge, Mbunge wa Mwibara lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania halina mabadiliko ya kisera na linaendelea kutekeleza kwa kiwango cha hali ya juu jukumu lake la kuwalinda raia na mali zao.

(b) Mheshimiwa Spika, matumizi ya mazoezi ya shabaha hayaathiri sheria inayolinda Hifadhi ya Taifa ndiyo maana Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linatumia eneo hilo.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa matumizi hayo ya mazoezi ya shabaha yameleta athari nyingi kwa wananchi wanaoishi kando kando ya Mlima Vunere. Sasa je, Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenda kwenye vijiji vilivyoko kandokando ya Mlima Vunele kujionea mazoezi hayo ya shabaha yalivyoleta athari kwa wananchi wa Vunere?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, eneo lolote linalotumika kwa shabaha halipitishwi kuwa eneo la matumizi hayo kabla ya utafiti wa kina na kitaalam kuhusu madhara yanayoweza kupatikana. Hata hivyo hakuna mtu makini anayeweza kukataa wito wa kuongozana na Mheshimiwa Kirigini. Niko tayari. (*Makofi/ kicheko*)

**SPIKA:** Huo sio umakini hata kidogo. Tuendelee na Mheshimiwa Charles Mwera. (*Kicheko*)

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la wananchi wa Mwibara linafanana sana na tatizo la wananchi wa Lonsoti katika Kata ya Tarime Mjini ambapo wanajeshi wamevamia ardhi na kuzuia wananchi wasilime, ambapo maeneo ya Jeshi ni maeneo ya Nyandoto. Je, ni lini sasa wanajeshi hao watarudi maeneo ya Nyandoto.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nirejee kwamba katika mazingira ya kawaida nchi yetu ndiyo nchi pekee ambayo inapenda kuwaita wanajeshi wake wanaotafuta maeneo ya kuwalinda wavamizi. Naomba tutumie hiyo fursa kila tunapoipata kuwapongeza askari wetu kwa kazi kubwa wanayoifanya kuwahangaikia wananchi.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mwera kwamba mimi na yeye kama ambavyo tumekuwa tukifanya tutaendelea kushirikiana kuona namna bora ambapo ulinzi wa Taifa letu unaimarishwa na wananchi wake wanapata maisha mazuri zaidi.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa suala hili limeoana sawasawa na wanajeshi kuvamia kijiji cha Cheju na kuweka bango sehemu ambazo wananchi muda mrefu wameshajiimarisha na kilimo zaidi ya miaka 30 nyuma. Hivi sasa wameweka mabango kwamba maeneo hayo yasitumike. Je, Waziri atatueleza nini ili wananchi wa Cheju waweze kuelewa madhumuni ya kuchukuliwa maeneo yao hadi kufika Unguja Ukuu Tindini?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo. Majeshi yetu yanatafuta maeneo kwa shughuli za kulinda Taifa letu, hayatafuti maeneo kwa shughuli za kibiashara wala kujinufaisha. Kwa vyovyote vile ni jambo la busara Wizara ya Ulinzi ikiendelea kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge katika kutatua maeneo ambayo yana migogoro. Kwa kweli tupo tayari, Mheshimiwa Mbunge anione tutashirikiana naye.

Na. 20

**Vigezo Vya Kujiunga na JKT**

**MHE. RAMADHAN A. MANENO (K.n.y. MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa Rufiji ina ardhi kubwa, nzuri na maji mengi:-

(a) Je, ni lini JKT watajenga kambi ya kilimo katika Bonde la Mto Rufiji hususan katika vijiji vya Nyamwage na Muhoro?

(b) Je, ni vigezo gani vinatumika (*Recruitment Criteria*) kujiunga na JKT ili kuleta usawa kwa Wilaya zote nchini?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia Mbunge wa Rufiji lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lipo tayari kuweka Kambi ya Kilimo katika Bonde la Mto Rufiji endapo Wilaya hiyo itatoa eneo kwa madhumuni hayo. JKT iko tayari kushirikiana na mamlaka husika katika kuainisha eneo linalofaa kwa ujenzi wa kambi hilo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu vigezo vinavyotumika kuwapata vijana wa kujiunga na JKT, JKT hutoa nafasi kwa mikoa yote nchini kwa kuzingatia wingi wa watu

waliopo katika kila mkoa. Baada ya JKT kugawa nafasi hizo mikoani, mikoa ndiyo hugawa nafasi kwenye Wilaya zake zote kwa kuzingatia kigezo hicho hicho cha wingi wa watu.

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vijana wetu wengi wanahitaji kujiunga na JKT na mara kwa mara wanapeleka maombi ya kujiunga lakini matatizo na utaratibu unaotumika si mzuri na unasababisha matatizo ya vijana wengi kutopata nafasi ya kujiunga na JKT na kwa kuwa Naibu Waziri amesema kigezo ni wingi wa watu mikoani. Je, haoni sasa wakati umefika kuangalia utaratibu mwingine unaofaa kuhakikisha vijana wetu wanapata nafasi za kutosha kujiunga na JKT?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, nashawishika kuamini kwamba nia ya Mheshimiwa Maneno ni kutaka nafasi za JKT ziongezwe ili tupate vijana wengi zaidi. Serikali italifanyia kazi ombi hilo.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Naulizia kuhusu kuweka *detach* pale kwenye barabara ya Ndundu-Somanga maana matatizo mengi ya ujambazi yanatokea pale. Je, si busara kwa Wizara kuweka *detach* angalau ya Jeshi la Kujenga Taifa pale ikaweza kufanya kazi hiyo ili kunusuru mali za wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu wa nchi yetu chombo kinachohusika na ulinzi wa ndani ya nchi yetu ni Jeshi la Polisi ambayo ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi yetu. Lakini inapotokea kwamba Mkoa unaohusika unaona haja ya kuongeza nguvu, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa inaweza kutoa maombi yake kwa Waziri wa Ulinzi ambaye atatoa maelekezo kwa Majeshi yetu kama ifaavyo. Kwa hiyo, nashauri Mkoa unaohusika kama unaona haja ya kuunda *detach* kwa ajili ya ulinzi kufuata utaratibu huo.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu tumetenga maeneo kadhaa, kwa mfano, Sanjaranda Kitaraka, Kirurumo Landani, ambapo Maafisa wa Jeshi walikuja wakakagua kwa nia ya kuanzisha Kambi ya Jeshi katika moja ya maeneo hayo. Sasa ni lini uamuzi huo utatolewa ili waje waanzishe Kambi katika maeneo hayo.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba Wizara yetu imeshafanya utafiti wa kutosha katika maeneo aliyoyataja na tunaendelea na mchakato tayari kuanzisha kambi katika eneo hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umepita na maswali yamekwisha. Navutiwa kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa majibu mafupi yanayolenga swali husika. Natumaini sehemu nyingi watakuwa wamesikia tangazo hilo pamoja na kule mabonde ya Wangoni.

Waheshimiwa Wabunge, tuna matangazo. Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Lucy Nkya ambao ni Ndugu Josephine Mmasi, Mwananchuo wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha Iringa na Ndugu Lucy Malya ni mwanafunzi wa Sekondari Mazinde Juu Lushoto, naomba wasimame, wale pale ahsanteni sana. Tunawatakia mafanikio katika masomo mema. Na uko kwenye shule nzuri sana hiyo.

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Mariam Kasembe ambaye ni Ndugu Hamza Omar toka Magereza Mbinga ambaye ni mwanawe Mheshimiwa Mbunge. Karibu sana. Matangazo mengine. Leo baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu yaani saa tano kuna semina muhimu sana inayohusu umuhimu wa mfumo wa utambuzi na usajili wa watu ambayo itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hii ni muhimu sana kwa wakati huu ambao tumeingia katika mfumo wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Lakini pia utaratibu ambao unawekwa kuhusu kusajili na kutoa vitambulisho wote ni ghali sana na gharama kubwa. Kwa hiyo ni vizuri tuweze kuhudhuria ili tuweze kuona undani wa mradi huu muhimu sana wa ulinzi wa Taifa letu kulinda demokrasia na hata kuangalia haki za Watanzania ili zisiweze kuporwa na watu wengine ambao si Watanzania.

Waheshimiwa Wabunge shughuli zilizopangwa kwa leo ndiyo zimefikia tamati, ahaa bado. Namwita sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya Hoja yake kuhusiana na kanuni zetu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nasimama hapa kwa heshima kutoa maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kwa kutumia Masharti yale ya Kanuni ya 150(1), Toleo la mwaka 2007. Kwa kuwa Mkutano wa Ishirini wa Bunge hili la Tisa wa kushughulikia Bajeti pamoja na shughuli zingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa kusikilizwa kwa muda wa siku 38 tu;

KWA KUWA muda huo umepangwa kwa kuzingatia umuhimu wa kupunguza muda kutoka siku 50 uliowekwa na kanuni ya 96 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007;

NA KWA KUWA muda huo unapunguzwa kutokana na sababu za msingi ya kuzingatia ratiba ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 unaotegemea kufanyika mwezi Oktoba, ratiba iliyotolewa na Tume ya Uchaguzi ambayo sambamba inaenda na uteuzi

wa Wagombea Ubunge hali ambayo inapelekea kuifanya ratiba ya Mkutano huu itoe muda wa kutosha kwa Serikali na kwa Vyama vya Siasa ili wakamilishe michakato ambayo imekwishaanza ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu utakaofanyika baadaye mwaka huu;

NA KWA KUWA baada ya kuzingatia sababu hiyo ya msingi Kamati ya Uongozi imeweka utaratibu utakaorahisisha uendeshaji wa shughuli za Bunge mahsusi kwa ajili ya kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/2011 yatakayowasilishwa kwenye Mkutano huu wa Ishirini wa Bunge;

NA KWA KUWA ili kuwezesha utaratibu huo kutumika wakati wa kupitisha Makadirio hayo ni lazima Bunge litengue Kanuni kadhaa zinazotumika kwa sasa kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni ile ya 150(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2010;

KWA HIYO BASI, Bunge sasa linaazimia kwamba kwa madhumuni ya Bunge kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2010/2011, Kanuni husika za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007, sdsa zitenguliwe katika maeneo manane kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 28(15), inayoeleza kwamba vikao vya Bunge vitafanyika siku zote za wiki isipokuwa Jumamosi, Jumapili au siku za mapumziko itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wenyewe ni:-

(i) Iwapo shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya kikao hazijamalizika, Spika atalihoji Bunge kuhusu Hoja ya Kuahirisha Kikao cha Bunge. Baada ya Hoja hiyo kuafikiwa, atakiahirisha Kikao hicho hadi siku inayofuata hata kama siku hiyo itakuwa ni Jumamosi, isipokuwa kwamba siku hiyo ya Jumamosi hakutakuwa na Kipindi cha Maswali.

(ii) Kanuni ya 96(7) inayoelekeza kwamba „muda wa kusoma Maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi na Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Hali ya Uchumi na Hotuba ya Bajeti kwamba utakuwa dakika zisizozidi 30 kwa kila hotuba, itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- Muda wa kusoma Maoni ya Kamati na yale ya Upinzani utakuwa dakika 20 kwa kila hotuba.

(iii) Kanuni ya 97(1) inayoelekeza kwamba Mjadala kuhusu hotuba ya Bajeti utaendelea kwa siku zisizozidi tano (5) ambapo dakika zisizozidi 15 zitatolewa kwa kila Mbunge anayetaka kuchangia Hotuba ya Bajeti itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- Mjadala kuhusu Hotuba ya Bajeti utaendelea kwa siku zisizozidi

tatu (3) ambapo dakika zisizozidi 10 zitatolewa kwa kila Mbunge anayetaka kuchangia Hotuba ya Bajeti.

(iv) Kanuni ya 99(6) inayoelekeza kwamba Waziri anapowasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yake atatumia muda usiozidi dakika 60, sasa itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- Isipokuwa Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, muda wa Waziri anayewasilisha Hotuba ya Makadirio ya Wizara yake utakuwa ni dakika zisizozidi 30.

(v) Kanuni ya 99(7) inayofafanua kwamba Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio ya Wizara husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wanapotoa maoni yao watatumia muda usiozidi dakika 30 kila mmoja, itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- (7) Waziri atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati iliyopitia Makadirio husika na Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambao watatoa maoni yao kwa muda usiozidi dakika 20 kila mmoja.

(vi) Kanuni ya 99(8) inayoeleza kwamba Mbunge anayejadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15, itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- Mbunge anayejadili Makadirio ya Matumizi ya Wizara mbalimbali ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 10.

(vii) Kanuni ya 99(9) inayoeleza kwamba Waziri Mtoa Hoja atapatiwa Muda usiozidi dakika 60 kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- Endapo Spika ataona kuwa, muda uliotengwa kwa ajili ya kujadili bajeti ya Wizara inayohusika umekaribia kwisha, atafunga mjadala ili kumpa Waziri Mtoa Hoja nafasi ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Wabunge wakati wa majadiliano kwa muda usiozidi dakika 30.

(viii) Kanuni ya 101(2) inayohusu mjadala katika Kamati ya Matumizi itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao sasa utumike:- (2) Mbunge yeyote anaweza kuomba ufafanuzi au maelezo zaidi katika kifungu chochote cha Fungu linalohusika wakati kifungu hicho kitakapofikiwa na Kamati ya Matumizi. (3) Mbunge atakayeomba ufafanuzi au maelezo kwa kutumia utaratibu huu, ataruhusiwa tu iwapo anataka ufafanuzi au maelezo ya ziada kuhusu jambo linalohusiana na kifungu husika na si kwa jambo la jumla na hataruhusiwa kuomba ufafanuzi au maelezo ya ziada kuhusu mambo mawili kwa wakati mmoja, isipokuwa kwa idhini ya Mwenyekiti. (4) Mbunge aliyepewa idhini na Mwenyekiti chini ya fasili ya (3) hapo juu atazungumza zaidi ya mara moja juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, hatimaye, kwa ajili ya umuhimu wa kauli hii, itabidi Waheshimiwa Wabunge wote wapate nakala na Ofisi yako itawapatia leo baadaye.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawahoji, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Uratibu na Bunge), kwa uchambuzi wa kina wa Kanuni zote ambazo zingeweza kuwa ni kipingamizi. Si jambo rahisi kuchambua kiasi hicho alichofanya. Kwa hiyo, inataka umakini. Asante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Hoja imetolewa ya kutengua Kanuni zetu Toleo la 2007 katika maeneo 8 kwa madhumuni ambayo Mheshimiwa Waziri ameyaeleza.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja zilizotolewa za Kuengua Kanuni Zilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Walioafiki wameshinda na kwa hiyo, Kanuni husika zitakuwa zimetenguliwa na naomba Katibu asaidie zigawiwe mara moja hizi nakala za maelezo haya ili zitusaidie kwa urahisi zaidi katika shughuli zetu za mijadala ya bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo ya tarehe 9 Juni ndiyo zimefikia tamati, kwa hiyo naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.30 Asubuhi, Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 10 Juni, 2010 Saa 3.00 asubuhi)*